**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

**KITUO CHA TAIFA CHA UBUNIFU NA TAARIFA ZA KIJIOGRAFIA (TNGC)**

# TANGAZO LA KUPOKEA MAOMBI YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI KWA MWAKA WA MASOMO 2026/2027

Kituo cha Taifa cha Ubunifu wa Teknolojia ya Kijiografia Tanzania (TNGC), ambacho ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kinawatangazia waombaji wenye sifa kuomba nafasi za kujiunga na programu zifuatazo za mafunzo ya kiufundi kwa mwaka wa masomo 2026/2027:

1. **Astashahada ya Upimaji ardhi kwa Ndege zisizo na Rubani (Drone) na Satelaiti ('*Drone Mapping and Satellite Surveying'*- NTA Ngazi ya 4)**

- **Muda wa masomo:** Mwaka mmoja wa masomo.

2. **Stashahada ya Upimaji Ardhi kwa Ndege zisizo na Rubani (Drone) na Satelaiti ('*Drone Mapping and Satellite Surveying'*- NTA Ngazi ya 5 & 6)**

- **Muda wa masomo:** Miaka miwili ya masomo.

3. **Astashahada ya Mfumo wa Taarifa za Kijiografia ('Geographical Information System'- GIS- NTA Ngazi ya 4)**

- **Muda wa masomo:** Mwaka mmoja wa masomo.

4. **Stashahada ya Mfumo wa Taarifa za Kijiografia ('Geographical Information System'- GIS- NTA Ngazi ya 5 & 6)**

- **Muda wa masomo:** Miaka miwili ya masomo

## MUHTASARI WA PROGRAMU

Programu hizi zinatoa mafunzo ya vitendo katika:

Uendeshaji wa ndege zisizo na rubani (Drones); Ukusanyaji wa taarifa za kijiografia; Uchambuzi wa picha za satelaiti na Mbinu za kisasa za upimaji ardhi.

Mafunzo haya yanawaandaa wahitimu kwa ajira na shughuli katika sekta za: Upimaji Ardhi; Uchoraji ramani; Usimamizi wa ardhi na Ufuatiliaji wa mazingira.

## SIFA ZA KUJIUNGA

A. **Astashahada ya Upimaji ardhi kwa Ndege zisizo na Rubani (Drone) na Satelaiti (NTA Ngazi ya 4)**

Mwombaji anatakiwa kuwa na angalau **ufaulu wa masomo manne (4)** katika Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE), kila somo likiwa na **daraja la D au zaidi**.

Masomo hayo lazima yajumuishe: Hisabati (Mathematics); na Jiografia (Geography).

Ufaulu katika masomo ya:

Fizikia (Physics) na Kiingereza (English Language), utazingatiwa kama **sifa ya ziada**.

**B. Stashahada ya Upimaji ardhi kwa Ndege zisizo na Rubani (Drone) na Satelaiti (NTA Ngazi ya 5 & 6)**

Mwombaji anatakiwa kuwa na mojawapo ya sifa zifuatazo:

**i.** Cheti cha Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE) chenye angalau **alama za ufaulu mbili** katika mojawapo ya masomo yafuatayo:
Fizikia; Jiografia; Hisabati; Kemi ana Sayansi ya Kompyuta au

**ii.** Astashahada ya Ufundi ya Msingi (NTA Ngazi ya 4) katika Drone Mapping and Satellite Surveying au programu nyingine inayohusiana na Upimaji Ardhi kutoka taasisi inayotambuliwa.

**C. Astashahada ya Mfumo wa Taarifa za Kijiografia - NTA Ngazi ya 4**

Mwombaji awe na Cheti cha Mtihani wa Elimu ya Sekondari [CSEE] na angalau Ufaulu wa alama 'D' nne 4, ambapo masomo mawili yawe kati ya: Jiografia, Hisabati, Fizikia, au Kemia.

**D. Stashahada ya Mfumo wa Taarifa za Kijiografia - NTA Ngazi ya 5 & 6**

Mwombaji anatakiwa kuwa na mojawapo ya sifa zifuatazo:

i. Cheti cha Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE) chenye angalau **alama za ufaulu mbili** katika masomo ya Hisabati, Jiografia, Biologia, Fizikia, au Kemia au
ii. Astashahada ya Ufundi ya Msingi (NTA Ngazi ya 4) katika fani ya Mfumo wa Taarifa za Kijiografia, Uchoraji Ramani, Usimamizi wa Ardhi, Uthamini na Usajili, Upimaji wa Ardhi, Photogrammetry, Geo-informatics, Mipangomiji, Usimamizi wa Mazingira, Geomatics, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, au Sayansi ya Kompyuta kutoka taasisi inayotambuliwa na NACTVET.

**JINSI YA KUOMBA**

1. Fomu za maombi zinapatikana kwa kupakuliwa kupitia tovuti ya Wizara: **www.lands.go.tz**
2. Fomu zilizojazwa kikamilifu ziambatanishwe na:

- Nakala zilizothibitishwa za vyeti au matokeo ya CSEE na/au ACSEE;
- Cheti cha kuzaliwa;
- Picha mbili (2) za hivi karibuni za pasipoti.

3. Maombi yatumwe kwa anuani ifuatayo:

**Mkuu wa Chuo,**
**Tanzania National Geo-Innovation Center (TNGC),**
**S.L.P. 1576,**
**Dodoma, au** Kwa barua pepe: **admissions.tngc@lands.go.tz**

**MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI**

Maombi yote yanapaswa kufikishwa **kabla au ifikapo tarehe 30 Agosti, 2026**.

**Imetolewa na:**

**Mkuu wa Chuo**
**Tanzania National Geo-Innovation Center (TNGC)**
**Dodoma, Tanzania**